**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA**

**SHULE YA SEKONDARI KWABASTOLA**

SHULE YA SEKONDARI KWABASTOLA
S.L.P. 20,
**MUHEZA**
Tarehe…………………..

***NAMBA ZA SIMU***
***MKUU WA SHULE-0713 681864/0768006836***
***MAKAMU MKUU WASHULE-0769753152***
***MATRON-0650816448***

**KUMB.NA.KWBTSS/F. V**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi

……………………………………………..

S.L.P …………………

...............

............

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KWABASTOLA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA MKOA WA TANGA MWAKA…………………………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka………………...na atasoma tahasusi ya…………………. Shule ipo umbali wa mita 500 kutoka barabara kuu itokayo SEGERA kuelekea TANGA mjini. Utashuka kituo cha mabasi maarufu kwa jina la KWABASTOLA. Usafiri kutoka hapo kituoni hadi shuleni ni TSH. 1,000/= kwa pikipiki (BODABODA).

Muhula wa Masomo unaanza tarehe……………….., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe………………………... Mwisho wa kuripoti ni tarehe………………………..

**2.** Mambo muhimu ya kuzingatia**:- (a)**

(i) Sare ya shule hii

**KWA WASICHANA** ni mashati mawili meupe ya mikono mirefu yasiobana na sketi mbili ***light blue*** ndefu mpaka karibu na viatu, zenye marinda ya kupanga

**KWA WAVULANA** mashati mawili meupe ya mikono mirefu yasiobana na suruali mbili za ***light blue*** za marinda zenye mifuko miwili mbele na mmoja nyuma kwa Wavulana isiyo ya kubandika.

(ii) Mashati mawili meupe ya mikono mirefu yasiyokuwa na urembo (nakshi) wowote.

(iii) Rangi ya Hijab ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

(iv) Sare ya Michezo ni trak suti 2 za rangi ***grey (kijivu)*** Kwa wasichana na trakisuti 2 rangi ***nyeusi*** kwa wavulana.

(v) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

(vi) oksi jozi mbili ***nyeupe*** kwa wasichana na ***nyeusi*** kwa wavulana.

(vii) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

(viii) Sweta rangi ya light blue, unaweza kuipata shuleni kwa (Tsh 15,000/=) ukiipenda.

(ix) Nguo za kushindia (*shamba dress*) kwa wasichana ni gauni la solo rangi ya ***brown (kahawia)*** kwa wanaotumia hijab rangi ya hijab ifanane na ya gauni. Kwa wavulana suruali ***brown (kahawia)*** na fulana (form six) rangi ya ***dark blue*** isiyo ya jezi;

(x) Tisheti(**T-shirt**) moja ya rangi ya ***grey(kijivu)***, unaweza kuipata shuleni Tsh 15,000/=) ukipenda.

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni ni:**

(i) Madaftari (*counter books Q4*) yasiopungua 10;

(ii) **Ream (A4)** ya Karatasi, Mbili (2) kwa mwaka;

(iii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*imeambatanishwa*);

(iv) Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

(v) Scientific Calculator;

(vi) Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na ukubwa wa futi tatu kwa sita.

(vii) Mashuka Jozi mbili, rangi ya ***light blue***, blanket 1, foronya, chandarua rangi ***nyeupe*** kwa wasichana na rangi ya ***blue*** kwa wavulana.

(viii) Nguo za ndani za kutosha;

(ix) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

(x) Ndoo mbili ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na kubwa moja kwa ajili ya kuhifadhia maji wakati wa shida.

**Vifaa vya usafi**

(i) Kwa wanafunzi wa CBG waje na soft broom 1, hard broom 1 na squizer 1

(ii) Kwa wanafunzi wa HGFa waje na reki 1, panga1 na toilet brush 1.

**(b) Michango mbalimbali**

**(i) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**FEDHA ZIINGIZWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE CRDB - 0150868257800, KWABASTOLA SECONDARY SCHOOL. Uje na slipy halisi ya benki yenye jina la mwanafunzi siyo nakala. HATUPOKEI FEDHA TASLIMU.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### (a) Sheria na Kanuni za Shule

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na

(ii) jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);

(iii) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

(iv) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

(v) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

(vi) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

(vii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

(viii) Kutunza mali za shule;

(ix) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

(x) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja

na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**(b) Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

(i) Wizi;

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo;

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;

(vii) Kufuga ndevu;

(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

(ix) Uvutaji wa sigara;

(x) Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba;

(xii) Kusababisha mimba;

(xiii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

(xiv) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa;

(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

(xviii) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

(a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

(b) Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

(d) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma Kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Karibu sana katika shule hii

Mkuu wa Shule

……….................................

**JUMA R. MDACHI**

**TANBIHI:**

Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. Tafadhali upatapo ujumbe wowote kuhusu mwanafunzi/mtoto wako usitume chochote, ni vema ukawasiliana na uongozi wa shule kupata ukweli wa taarifa husika kwa namba zifuatazo: -

- Mkuu wa shule -0713681864/0768006836
- Makamu Mkuu wa Shule -0769753152

Jina la Mwanafunzi…………………………………..………,

S.L.P …………,

Terehe………………,

**Mkuu wa Shule,**

Shule ya Sekondari Kwabastola,

S.L.P. 381, Muheza.

PICHA YAKO HAPA

Yah: **UCHAGUZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO……………………**

1. Ahsante sana kwa barua yako yenye kumb. SNSS/24/…………….……….. tarehe…. …. ……..……… Ya kunijulisha kuwa nimechaguriwa kujiunga na kidato cha tano shuleni hapo.
2. Ninatoa ahadi kutii sheria zote za shule ambazo nimezisoma na kuzielewa.
3. Endapo nitakutwa na simu shuleni nitakuwa nimejifukuzisha shule kwa mujibu wa sharia
4. Ninakubali/ sikubali nafasi hii niliopewa na taifaNikotayari kutimiza maagizo yote niliopewa ya kujiunga na shule hii.

**Historia fupi ya Mwanafunzi husika**

| Jina kamili uliloandikishwa shuleni | Shule ya msingi na sekondari ulizopitia | Tarehe ya kuzaliwa | Mahali ulipozaliwa | Dini/Dhehebu lako | URAIA |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Msingi** | | | | |
| | | | | | |
| | **Secondary** | | | | |
| | | | | | |

Nakiri kuwa maelezo yote niliotoa hapo juu ni sahihi

Jina la mwanafunzi…………………………………..…Sahihi…………………Tarehe…………...…..

**SEHEMU YA MZAZI/ MLEZI KUKUBALI KUCHAGULIWA KWA MWANAFUNZI HUSIKA.**

Jina la Mzazi/ Mlezi ………………………………………………

Kazi ………………………..…….

Namba ya simu ya Mzazi/ Mlezi: ………………………………… S.L.P...………..............

Nakiri kuwa huyu ni mwanangu. Nakubali/sikubali nafasi hii aliyopewa ya kujiunga na shule hii. Nakubaliana/Sikubaliani na sheria na maagizo yote ya shule aliyopewa ya kujiunga na shule hii. Naahidi kumhudumia mwanangu kikamilifu na kushirikiana na uongozi wa shule katika kufanikisha maendeleo ya elimu yake.

**Endapo mwanangu atakutwa na simu shuleni afukuzwe shuleni kwa mujibu wa sheria ya shule.**

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ………………………..

Tarehe ………..….

**PICHA YA MZAZI**

**KWABASTOLA SECONDARY SCHOOL,**

**P.O.BOX 20, MUHEZA,**

**DATE: ………………..**

REF NO: SNSS/21/MED. ………………..

## SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

TO THE MEDICAL OFFICER

……………………………………………………

……………………………………………………

Name of student: …………………………………………………………………………...

Form …………………………… Term …………………………. Year …………………

Please kindly examine the above named student to prove his/ her fitness undertaking studies at our school.

1. X- Ray ( )   2. Urine ( )   3. Stool ( )
4. Physical fitness ( )   5. V.D ( )   6. Tuberculosis ( )

**A: (I) PRELIMINARY INFORMATION (BY THE STUDENT BEFORE THE DOCTOR)**

| N0 | DISEASE | YES/NO | NO | DISEASE | YES/NO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | 10 | Epilepsy | |
| 2 | Pneumonia | | 11 | Ear/Nose and threat | |
| 3 | Asthma | | 12 | Skin disorder disease | |
| 4 | Heart trouble | | 13 | Anaemia | |
| 5 | Recurrent indigestion | | 14 | Operations | |
| 6 | Jaundice | | 15 | Serious Accident | |
| 7 | Dysentery | | 16 | Malaria | |
| 8 | Kidney and urinary trouble | | 17 | Stomach trouble | |
| 9 | Nervous breakdown | | 18 | Eye disorder | |

**(II) VACCINATIONS AND INNOVULATIONS HISOTRY**

| DISEASE | 1ST DATE | 2ND DATE | 3RD DATE |
|---|---|---|---|
| Small pox | | | |
| Whooping cough | | | |
| Measles | | | |
| Yellow fever | | | |
| Cholera | | | |

**B: MEDICAL EXAMINATION REPORT**

(a) Weight (b)

Heart beat (c)

Vision etc.

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above and consider that he/she is physically fit/unfit to undergo studies

DOCTOR'S NAME & SIGNATURE

……………………………………………………………………………………………….

DATE ……………………. AND STAMP…………….